



63 Kifo cha Sauli

Maswali

1. Nani alikuwa akipigana na Waisraeli?
2. Mbona Mungu hakuwa akisaidia Sauli?
3. Nani alishinda vita?
4. Wafilisti walipigana na Sauli na wanawe wakiwa wapi?
5. Nini ilifanyika kwa Yonathani na wana wengine wa Sauli?
6. Sauli alipoumizwa, aliambia mtu wake wa kubeba silaha afanye nini?
7. Sauli alikufa namna gani?
8. Wafilisti walifanya nini kwa miili ya Sauli na wanawe?
9. Watu wa Yabesh-Gileadi walifanya nini?
10. Daudi alienda kuishi wapi?

Majibu

1. Wafilisti walipigana na Waisraeli.
2. Sauli alikuwa amemwacha Mungu na hakumtii.
3. Wafilisti walishinda vita.
4. Walipigania kwa mlima wa Gilboa.
5. Yonathani na wana wengine wa Sauli waliuawa.
6. Sauli aliambia mtu wa kumbebea silaha amuue na upanga wake.
7. Sauli aliangukia upanga wake na akajiwa mwenyewe.
8. Wafilisti walitundika miili ya Sauli na wanawe kwa ukuta huko Beth-shani
9. Watu wa Yabesh-Gileadi walichukua miili na kuenda kuzika.
10. Daudi alienda kuishi Hebroni.

Kwa Biblia

1 Samweli milango wa 31 na 2 Samweli 1:17—27

Kiini cha somo

Kuonyesha kwamba Mungu hakuwa na Sauli kwa sababu Sauli hakumtii Mungu na tena alifanya maovu mengi. Watu waovu wanaweza kuwa vizuri kwa muda, lakini mwishowe wanaenda kaburini na maisha yao yanakwishia hapo milele

Somo

Sauli alikuwa Mfalme muovu. Alikuwa na maringo tena hakutii amri za Mungu. Sauli alimchukia Daudi. Alijua kwamba Mungu alikuwa amemchagua Daudi kuwa Mfalme baadaye. Sauli alijaribu kuuu Daudi. Mungu alimweka Daudi salama kwa sababu Daudi alimwamini. Mungu hakuwa akimsaidia Sauli kwa sababu alikuwa amemwacha.

Wafilisti walikuwa adui wa Waisraeli. Walikuja kupigana na Waisraeli. Sauli aliogopa sana kwa sababu alijua Mungu hakuwa akimsaidia tena.

Wafilisti walienda kupigana na Waisraeli. Wafilisti walikuwa na nguvu kuliko Waisraeli. Walikuwa na silaha za nguvu na magari na farasi. Mungu hakuwa anasaidia Sauli na Waisraeli. Wafilisti walishinda vita. Waisraeli wengi waliuawa. Waisraeli walitoroka.

Wafilisti walifukuza Waisraeli. Waliwafukuza mpaka mlima wa Gilboa. Kulikuwa na vita vikali sana kwa mlima wa Gilboa na Waisraeli wengi waliuawa.

Wafilisti walitaka kuwashika Sauli na wanawe. Sauli alikuwa ndiye Mfalme. Ikiwa watashika Mfalme pamoja na wanawe, basi, Waisraeli hawatakuwa na kiongozi. Wafilisti waliua wana watatu wa Sauli kwa mlima wa Gilboa. Kwa hivyo Yonathani aliuawa.

Sauli aliumizwa na mishale za Wafilisti. Sauli alijua kwamba atakufa. Sauli aliogopa kwamba Wafilisti watamchukua. Watamfanyia dhihaka na kumteza. Wafilisti walikuwa wamemkaribia sana. Sauli hakuwa na nguvu za kutoroka. Sauli aliambia mbeba silaha zake amue kwa upanga wake. Lakini mbeba silaha aliogopa. Hangeweza kuu Sauli. Kwa hivyo Sauli alichukua upanga wake. Aliangukia upanga na kujiua.



Wafilisti walipata miili ya Sauli na wanawe. Walichukua hizo miili kwa mji wa Beth-shani. Walitundika miili za Sauli na wanawe kwa ukuta huko Beth-shani. Walifurahi kwa sababu walikuwa wameshinda Waisraeli. Walifanya mzaha kwa miili za Sauli na wanawe.


Mwanzoni Sauli alipokuwa Mfalme, aliokoa maisha ya watu wa mji wa Yabesh-Gileadi. Watu wa Yabesh-Gileadi walikuwa na heshima kwa Sauli. Watu wa Yabesh-Gileadi walikasirika sana waliposikia kwamba Wafilisti walikua wametundika miili za Sauli na wanawe kwa ukuta kule Beth-shani. Walisafiri usiku wote wakienda Beth-shani. Waliiba miili ya Sauli pamoja na wanawe kutoka kwa Wafilisti. Walichukua hizo miili na kuzirudisha Yabesh-Gileadi. Walizika miili ya Sauli na wanawe chini ya mti.

Daudi alisikia kwamba Sauli na wanawe walikua wamekufa. Daudi alirarua nguo zake. Daudi na watu wake walilia na kuomboleza kwa ajili ya Sauli na wanawe. Siku hiyo hawakula chakula kwa sababu walikuwa na uchungu.

Daudi alitumia watu wa Yabesh-Gileadi habari. Aliwashukuru kwa ujasiri wao wa kuenda na kuchukua miili ya Sauli na wanawe. Aliwashukuru kwa kuzika Sauli na wanawe kwa njia ya heshima.

Daudi aliandika wimbo wa maombolezo kuhusu kifo cha Sauli na Yonathani mlimani wa Gilboa.

*Sauli na Yonathani
kwa uhai wana upendo na ni wazuri,
na kwa kifo hawakuachana.
Walikuwa wepesi kuliko tai,
na nguvu kuliko simba.
Mashujaa waliangukaje kwa vita!
Ninakuhuzunikia wewe, Yonathani.
Upendo wako kwangu, waajabu.
Mashujaa waliangukaje!
Silaha za vita zimeangamia!*



Silaha za vita

Daudi hakuhitaji kutoroka kutoka kwa Sauli tena. Daudi alienda kuishi Hebroni. Alitawazwa kuwa Mfalme. Kila mara Daudi alijaribu kumpenda Mungu na kumtii. Alikuwa Mfalme mzuri sana.